Toleo 77 - Dhul Qa'adah 1444 H / Juni 2023 M

# UQAB
Jarida la

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**
Utozaji Ushuru Sura ya Kikatili ya Ubepari

**HABARI NA MAONI**
Chini ya Mfumo Uliofeli wa Kirasilimali, Wakristo Wanakuwa Mawindo Rahisi ya Wahalifu

**MATOLEO**
Wanawake wa Kiislamu nchini Iraq walio katika Mgomo wa Njaa Hawana Msaidizi

**JIBU LA SWALI**
Tofauti Kati ya Manabii na Mitume, Amani Iwe Juu Yao



## Tanzia ya Mbebaji Ulinganizi

Taarifa kwa Vyombo Vya Habari

# Utozaji Ushuru Sura ya Kikatili ya Ubepari

Wakenya wanapambana na nyakati ngumu zaidi juu ya mapendekezo ya Sheria ya Fedha ya 2023. Mswada wa fedha uliowasilishwa bungeni unaregesha asilimia 16 ya ushuru wa ongezeko la thamani (VAT) kwa bidhaa za petroli pamoja na kuanzisha ushuru wa nyumba wa asilimia 3. Bei za takriban bidhaa na huduma zote zimepanda katika miezi ya hivi karibuni ikiwa ni pamoja na gharama ya umeme, mafuta na unga wa mahindi.

**Sisi katika Hizb ut Tahrir / Kenya tungependa kufafanua yafuatayo:**

Mswada huo umefichua unafiki wa wanasiasa ambao hawana ikhlasi huku maafisa wakuu wa serikali wa sasa wakikataa Mswada wa Marekebisho wa Bidhaa za Petroli (Ushuru na Kodi) wa 2021 katika utawala uliopita. Huku Serikali ya Jubilee ikiwa nje ya afisi, waliokuwa wapinzani wa wakati huo wa ushuru wa juu ndio sasa wanaouunga mkono zaidi.

Kwa mtazamo wa harakaharaka wa utozaji ushuru mkubwa kwa Wakenya wa kawaida wakati wa kabla na baada ya uhuru haujawahi kutatua matatizo yoyote ya kiuchumi na kifedha bali kuitumbukiza nchi katika mgogoro wa kudumu wa kiuchumi na kifedha. Inavyoonekana, utozaji ushuru kama pato kuu katika mfumo wa kibepari haujakuwa na kamwe hautakuwa suluhisho kwa uchumi ambao tayari unaugua.

Imedhihirika wazi kuwa serikali za kibepari hazijitwiki jukumu katika kusimamia mambo na maslahi ya mwananchi wa kawaida. Badala yake, kinacho maanishwa na kuboresha maisha ya watu wake ni kuongeza kodi ambayo hatimaye huathiri kupanda kwa bei za bidhaa na huduma na kusababisha umaskini uliokithiri. Kuongeza chumvi kwenye kidonda, tawala za kibepari zinategemea sana ukopaji fedha. Kuchukua mikopo mingi kwa kodi za wananchi kama dhamana ya kufadhili miradi 'hewa' kisha baada ya hapo fedha hizo zinaporwa na viongozi walafi wa juu serikalini.

Tunasisitiza tena kwamba Dola ya Khilafah inayotabikisha mfumo wa kiuchumi wa Kiislamu ulio huru kutokana na utozaji kodi zote za kikatili kama vile VAT na Kodi ya Mapato. Mtume Muhammad (saw), amesema;

**«لَا يَدْخُلُ الْجَنَّةَ صَاحِبُ مَكْسٍ» "Mtoza ushuru hataingia peponi."** (Ahmad). Uislamu una mfumo wake wa kipekee wa ukusanyaji mapato, ikiwa ni pamoja na mapato kutoka kwa mali ya umma (kama vile gesi) na uzalishaji wa kilimo (kama vile kharaj), ambayo huingiza mapato bila kunyonga shughuli za kiuchumi. Na mfumo wa kiuchumi wa Kiislamu unaorodhesha rasilimali kama vile nishati, ardhi ya malisho na maji kama mali ya umma. Dola wala watu binafsi hawawezi kujinyakulia manufaa yake peke yao, badala yake manufaa kutoka nazo ni kwa ajili ya watu wote. Mtume Muhammad (saw), amesema:

«الْمُسْلِمُونَ شُرَكَاءُ فِي ثَلَاثٍ الْمَاءِ وَالْكَلَإِ وَالنَّارِ»

**"Waislamu ni washirika katika vitu vitatu: maji, malisho na moto" (Ahmad, ibn Majah)**

**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari wa Hizb ut Tahrir, Kenya**

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Wilayah Jordan**

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

KUMB: 21/1444 Alhamisi, 28 Shawwal 1444 H 18/05/2023 M

# Tanzia ya Mbebaji Ulinganizi

**مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ فَمِنْهُم مَّن قَضَى نَحْبَهُ وَمِنْهُم مَّن يَنتَظِرُ وَمَا بَدَّلُوا تَبْدِيلاً**

## “Miongoni mwa Waumini wapo watu walio timiza waliyo ahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo.” [Al-Ahzab:23]

Kwa imani na kujisalimisha kwa qadhaa ya Mwenyezi Mungu (swt), Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir/Wilaya ya Jordan inaomboleza kwa Waislamu kwa jumla, na watu wa Jordan na Waislamu hasa wa Australia, mmoja wa wanachama wanyoofu, wenye subira na waheshimika wa hizb, mwenye misimamo imara yenye kumridhisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake (saw), na sisi hatumtakasi yeyote mbele ya Mwenyezi Mungu.

**Mwanafikra wa kisiasa kutoka kizazi cha zamani cha wanachama wa Hizb ut Tahrir**

**Mhandisi Ismail Al-Wahwah (Abu Anas)**

Ambaye alifariki dunia kwa rehema za Mwenyezi Mungu (swt) mnamo siku ya Jumatano, 27 Shawwal 1444 H sawia na 17/5/2023 M, nchini Australia, baada ya maisha yake aliyoishi katika utiifu kwa Mwenyezi Mungu (swt) akibeba ulinganizi wa haki na kheri pamoja na Hizb ut Tahrir, ikifanya kazi ya kuregesha maisha kamili ya Kiislamu kupitia kusimamisha Dola ya Khilafah kwa njia ya Utume, kwa subira licha ya mashtaka mengi na kukamatwa kwake, vifungo vya jela mara kadhaa, na hukmu za kidhalimu ambazo ubatili wake umethibitika, kama ilivyo katika ile kesi iliyozuliwa inayoitwa “Mu’ta”, alitafuta malipo yake kutoka kwa Mwenyezi Mungu, akitegemea nusra Yake (swt), licha ya yale aliyokumbana nayo na kuteseka wakati wa maradhi yake.

Yeye, Mwenyezi Mungu amrehemu, alibaki imara juu ya haki aliyoibeba, mkaidi na muwazi. Alikuwa akiendelea, azma yake haikupungua, alitangaza haki kwa hotuba zake za kijasiri na mahojiano ya kisiasa ya vyombo vya habari. Alionyesha imani juu ya ahadi ya Mwenyezi Mungu (swt) kwa Ummah wa Uislamu ya ushindi na tamkini na kusimamishwa kwa Dola ya Khilafah Rashida kwa njia ya Utume, ambayo daima imekuwa ndio lengo la wito wake na uhamasishaji wa Ummah.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu amrehemu maiti wetu, maiti wa Ummah, kwa rehema zake, na amkubalie kwa mapokezi mema, na ayajaalie makaazi yake kuwa Firdaus ya juu kabisa Peponi pamoja na manabii, wakweli, mashahidi, watu wema, kwani wao ndio wandani bora, na kumlipa kwa niaba yetu na Uislamu na Waislamu malipo bora zaidi. Na tunamuomba (swt) kwa ajili yetu na jamaa zake, subira, faraja, na rambirambi njema.

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

**katika Wilayah Jordan**

# HABARI NA MAONI

# Chini ya Mfumo Uliofeli wa Kirasilimali, Wakristo Wanakuwa Mawindo Rahisi ya Wahalifu




Habari:

Polisi wa Kenya walimkamata mwinjilisti wa televisheni wa Kenya mwishoni mwa Aprili, 2023 na kufikishwa mahakamani Ijumaa tarehe 28 Aprili 2023 baada ya ripoti za "mauaji ya halaiki ya wafuasi wake," Waziri wa Mambo ya Ndani Kithure Kindiki alisema, huku mamlaka zikichunguza vifo vyengine vingi vinavyohusishwa na ibada za kundi la kidini kutoka eneo hilo hilo. Huku habari za kuzuiliwa kwa Mchungaji Ezekiel Odero zikienea, maafisa walisema idadi ya waliouawa Shakahola sasa imefikia 110 katika uchunguzi wa kundi tofauti la kidini ambao umelishtua taifa na kusababisha wito wa kufanywa msako kwa makundi ya kidini.

**Maoni:**

Ulimwengu unapoamka na habari hizi za kutisha, idadi ya miili iliyofukuliwa hadi sasa ni zaidi ya 110 huku watoto wakiwa ndio wengi wa waliofariki. Watu wengi wanaanza kujiuliza ni kwa jinsi gani watu wanaweza kufikia kiwango hiki cha kufa kwa njaa ikiwa ni pamoja na watoto wao wachanga kwa imani ya "kukutana na Yesu" au kitu chengine kilichopangwa ambacho kingeweza kuwa sababu ya uhalifu huu wa kinyama. Ama kuhusu sababu ya pili ni njama zaidi kuliko uhalisia, kwa sababu nyepesi ya madhehebu katika Jumuiya ya Wakristo ya aina hiyo ambapo wafuasi wanauawa kwa wingi ili kuamini kupata uzima wa milele ilitokea katika historia yake yote.

Ili kuwa na utambuzi bora wa tukio hili la kusikitisha na lisilo stahiki, lazima tujizungushe na uhalisia wote ikiwemo hali ya kijamii na kisiasa ambayo imewezesha hili. Siasa inafafanuliwa kuwa ni sayansi ya kudhibiti uhusiano wa kibinadamu na yote yanayotokana na uhusiano huu ikiwa ni pamoja na mihemko k.m., furaha, huzuni, simanzi, msongo wa mawazo na fahamu kama matumaini n.k. Leo matumizi mabaya ya dawa za kulevya na ulevi yanaongezeka kama vile mzazi mmoja katika familia malezi ya watoto, na vilevile ongezeko la umaskini na ukosefu wa ajira unaoambatana na kufeli kwa uongozi wa kisiasa kama ilivyo kufeli kwa idara ya mahakama. Kwa maneno mepesi mfumo wa kiitikadi (URASILIMALI) uvurugika na wanadamu wametumbukia katika dimbwi la ukosefu wa matumaini na hatimaye kuwa mawindo ya wahalifu waliojigeuza kuwa "WATU WA MUNGU".

Pia, hii inaonyesha itikadi ya Kikristo haiafikiani na umbile la mwanadamu, yaani, ukosefu wa uongofu na kugongana na umbile la mwanadamu. Uislamu ndio itikadi pekee inayoafikiana na umbile na akili ya mwanadamu. Mfumo wa Kiislamu humuongoza mwanadamu kuishi chini ya sheria za Mola wa Rehema ambazo ziko ndani ya mipaka ya uwezo wa mwanadamu. Mfumo unaomuepusha mwanadamu na madhara na maovu yanayoweza kuanguka katika maisha yake.

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ

**“Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.” [Al-Anbiya: 107]**

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ali Omar**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

# Wanawake wa Kiislamu nchini Iraq walio katika Mgomo wa Njaa Hawana Msaidizi Chini ya Sheria za Kibepari za Kiliberali

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Imrana Mohammad**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

Mnamo tarehe 6 Mei 2023, BBC iliripoti kuwa mamia ya wanawake wamegoma kula katika gereza moja la Iraq katika mji mkuu wa Baghdad. Wanapinga kuzuiliwa kwao kwa kuwa sehemu ya kundi la Dola ya Kiislamu, baada ya kile wanachosema kuwa ni kesi zisizo za haki. Kundi hilo linasemekana kujumuisha raia wa kigeni kutoka Urusi, Uturuki, Azerbaijan, Ukraine, Syria, Ufaransa, Ujerumani na Marekani. "Inafikiriwa kuwa takriban watoto 100 pia wanazuiliwa katika kituo hicho".

Hofu za ile iliyokuwa Iraq zinazidi kuwa mbaya zaidi kwa wanawake na watoto katika eneo hilo. Mshtuko usio na kifani ambao ni lazima upitiwe na mtoto aliyefungwa gerezani ni jinamizi la kutisha. Kwa bahati mbaya, kwa sera za kikoloni za Kibepari kutawala ardhi zetu, hakuna njia ya kumaliza uhalisia huu wa kikatili. Wanawake na watoto wanatumiwa kama mifano ya kuwaadhibu na kuwafundisha Waislamu wengine kwamba kutakuwa na adhabu kubwa kwa wale watakao jaribu kupinga utawala wa Magharibi.

Hakuna Dola ya Kiislamu popote pale duniani. Ni ukweli ambao Magharibi inaujua waziwazi. Yale yanayotokea kwa mfano wa wanawake na watoto hawa ni ugaidi tu chini ya bendera ya kulinda uhuru. Kutia hofu katika akili za Waislamu endapo watataka kushikamana na kitambulisho chochote wa Kiislamu ndilo lengo la kweli hapa.

Waislamu wa ulimwengu wanaweza tu kutarajia aina hizi za unyanyasaji kurefushwa na kuharakishwa kadiri kazi kwa ajili ya Khilafah ya kweli kupitia Hizb sahihi kupatikana kwake inavyozidi kuwa karibu.

Tangu 2017, maelfu ya wanawake na watoto wamewekwa kizuizini. Baadhi waliregeshwa katika mataifa yao, lakini wengi wamesalia katika jela za Syria na Iraq. Haki za binadamu kama zilivyojadiliwa katika sheria za Umoja wa Mataifa hazitumiki katika kesi za Waislamu, lakini lengo lao la kindoto kama chombo cha kuweka udhibiti liko wazi katika kesi hii ya ukandamizaji.

Maneno ya Mwenyezi Mungu (swt) yanapatikana tunapoonywa juu ya hatari kubwa tunazokabiliana nazo kama Umma wakati mambo yetu yapo mikononi mwa adui anayetaka kuiangamiza Quran na Sunnah kama marejeo katika siasa za dunia.


**يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَتَّخِذُواْ عَدُوِّى وَعَدُوَّكُمْ أَوْلِيَآءَ تُلْقُونَ إِلَيْهِم بِٱلْمَوَدَّةِ وَقَدْ كَفَرُواْ بِمَا جَآءَكُم مِّنَ ٱلْحَقِّ يُخْرِجُونَ ٱلرَّسُولَ وَإِيَّاكُمْ ۙ أَن تُؤْمِنُواْ بِٱللَّهِ رَبِّكُمْ إِن كُنتُمْ خَرَجْتُمْ جِهَـٰدًا فِى سَبِيلِى وَٱبْتِغَآءَ مَرْضَاتِى ۚ تُسِرُّونَ إِلَيْهِم بِٱلْمَوَدَّةِ وَأَنَا۠ أَعْلَمُ بِمَآ أَخْفَيْتُمْ وَمَآ أَعْلَنتُمْ ۚ وَمَن يَفْعَلْهُ مِنكُمْ فَقَدْ ضَلَّ سَوَآءَ ٱلسَّبِيلِ** **“Enyi mlio amini! Msiwafanye adui zangu na adui zenu kuwa marafiki mkiwapa mapenzi, na hali wao wamekwisha ikataa haki iliyo kujieni, wakamfukuza Mtume na nyinyi kwa sababu mnamuamini Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wenu. Mnapotoka kwa ajili ya Jihadi katika Njia yangu na kutafuta radhi yangu, mnafanya urafiki nao kwa siri, na Mimi nayajua mnayo yaficha na mnayo dhihirisha. Na mwenye kufanya hayo kati yenu basi ameipotea njia ya sawa.”** [Al-Mumtahina 60;1]

Video zilizotumwa kwa BBC ya Kiarabu kutoka ndani ya jela la Baghdad zinaonyesha wanawake waliodhoofika wakiwa wamelala kwenye sakafu ya mawe magumu. Inadhaniwa kundi hilo halijala tangu tarehe 24 Aprili.

BBC imeambiwa kwamba mwanzoni mwa mgomo huo wa njaa, washiriki walikuwa wakinywa nusu glasi ya maji kwa siku. Baadhi ya wanawake sasa wameacha kunywa kabisa.

Watoto wadogo pia wanaweza kuonekana kwenye kanda hiyo ya video - wengi wanaripotiwa kuzaliwa ndani ya jela hilo.

Mwenyezi Mungu (swt) airegeshe hadhi ya Ummah huu katika hali yake ya awali kabla ya kuvunjwa Khilafah, Amin!



JIBU LA SWALI

# Tofauti Kati ya Manabii na Mitume, Amani Iwe Juu Yao

**Swali:**

Assalam Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh

Katika kitabu, Shakhsiya ya Kiislamu, sehemu ya kwanza ya sura ya Manabii na Mitume, ukurasa wa 130, inasema:

“Kwa hivyo, Musa (as) alikuwa Nabii kwa sababu alipewa wahyi na Shari’ah na Mtume kwa sababu Shari’ah hii ilikuwa kwa ajili ya utume wake. Kwa upande mwingine, ingawa Harun (as) pia alikuwa ni Nabii kwa sababu alipewa wahyi na Shari´ah, hakuwa Mtume kwa sababu Shari´ah iliyoteremshwa kwake haikuwa kwa ajili ya utume wake, bali ilikuwa kwa ajili ya utume wa Musa (as)”.

Tutaunganisha vipi baina ya yale yaliyotajwa katika kitabu, Shakhsiya ya Kiislamu, na yale yaliyothubutu katika Kitabu (Qur’an) pindi Mwenyezi Mungu (swt) anaposema: فَأْتِيَاهُ فَقُولَا إِنَّا رَسُولَا رَبِّكَ **“Basi mwendeeni, na mwambieni: Hakika sisi ni Mitume wa Mola wako Mlezi!”** [Ta-Ha: 47] فَأْتِيَا فِرْعَوْنَ فَقُولَا إِنَّا رَسُولُ رَبِّ الْعَالَمِينَ **“Basi mfikieni Firauni na mwambieni: Hakika sisi ni Mitume wa Mola Mlezi wa walimwengu wote.”** [Ash-Shu’ara: 16] Katika tafsiri zote yeye ni Mtume na Nabii.

**Jibu:**

Wa Alaikum Assalam Wa Rahmatullah Wa Barakatuh

**Kwanza: Kumekuwa na ikhtilafu baina ya wanazuoni kuhusiana na tafauti baina ya Nabii na Mtume katika kauli kadhaa, zikiwemo:**

1- Nabii ni yule anayeteremshiwa kazi (taklif) na wala haamrishwi kuifikisha. Akiamrishwa kuifikisha basi ni Mtume. Imeelezwa katika Fath Al-Bari na Ibn Hajar Al-Asqalani: [Fath Al-Bari cha Ibn Hajar (11/112)

Neno ‘Unabii’ na ‘Ujumbe’ ni tofauti kiasili. Unabii unatokana na naba’ (julisha), ambayo ni habari. **Nabii katika desturi za kawaida ni yule aliyepewa habari na Mwenyezi Mungu kwa amri inayohitajia kazi, lakini akiamrishwa kuifikisha kwa wengine, basi yeye ni Mtume; vyenginevyo, yeye ni Nabii si Mtume.** Na kwa kuzingatia hili, kila Mtume ni Nabii lakini sio kinyume chake. Nabii na Mtume wanashiriki jambo la jumla ambalo ni habari (naba'), na wametengana katika ujumbe, hivyo ukisema fulani na fulani ni Mtume, unamaanisha kuwa yeye ni Nabii na Mtume. Ukisema fulani na fulani ni Nabii, basi haimaanishi kuwa yeye ni Mtume...]

2- Mtume ni yule aliyetumwa kufikisha wahyi na kwake kuna Kitabu, na Nabii ni yule aliyetumwa kufikisha wahyi kwa ujumla. Al-Ainy ametaja yafuatayo katika “Al-Banaya Sharh Al-Hidaya”: [Al-Banaya Sharh Al-Hidaya (1/116) [... Basi tafauti baina ya Mtume na Nabii: **Mtume: ni yule aliyetumwa kufikisha wahyi na kwake kuna Kitabu, na Nabii ni yule aliyetumwa kufikisha wahyi kwa ujumla, sawa ilikuwa pamoja na Kitabu au bila Kitabu,** kama Yoshua, amani iwe juu yake, kwa hivyo Nabii ni mkuu kuliko Mtume. Hivi ndivyo alivyosema Sheikh Qawam al-Din al-Atrazi katika “Sharh” yake, na katika hilo alimfuata mtunzi wa “Al-Nihaayah” pale aliposema: Mtume: ni Nabii ambaye ana Kitabu pamoja naye, kama Musa (as), na Mtume: ni mwenye khabari za Mwenyezi Mungu, hata kama hana Kitabu, kama Yoshua, amani iwe juu yake. Mtume (saw) amesema: عُلَمَاءُ أُمَّتِي كَأَنْبِيَاءِ بَنِي إِسْرَائِيل **“Wanachuoni wa Ummah wangu ni kama Manabii wa wana wa Israili,”** wala hakusema: “Mitume wa Israili.” Sheikh Akmal al-Din, Mwenyezi Mungu amrehemu, akawafuata na akawapambanua hivi].

3- (Mtume ni yule aliyeteremshiwa Shariah na ameamrishwa kuifikisha, huku Nabii ni yule aliyeteremshiwa Shariah ya Mitume wengine na ameamrishwa kuifikisha. Mtume ni yule mwenye kuamrishwa kufikisha Shariah iliyoteremshwa kwake, na Nabii ni yule aliyeamrishwa kufikisha Shariah za wengine), na hii ndiyo rai tuliyoichagua na kuibainisha katika kitabu “Shakhsiya ya Kiislamu”, juzuu ya 1, ukurasa wa 35-38 nakala ya Word:

[**Manabii na Mitume:** Nabii na ‘Mtume’ (rasul) ni maneno mawili yanayotofautiana lakini yanashirikiana katika upande kwamba Sharia inateremshwa kwa wote wawili. Tofauti kati ya Mtume na Nabii ni kwamba wa kwanza amepewa wahyi kwa Shari’ah ambayo ameamrishwa kuieneza, huku wa pili, yaani Nabii, pia amepewa wahyi, lakini ameamrishwa kueneza Shari’ah ya Mitume. Kwa maana nyengine, Mtume ameamrishwa kueneza Shari’ah yeye mwenyewe, huku Nabii anaeneza Shari’ah ya Mitume. Qadi al-Baydawi katika ufafanuzi wa kauli ya Mwenyezi Mungu (swt), وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ وَلَا نَبِيٍّ **“Na hatukumtuma kabla yako Mtume wala Nabii,”** [Hajj: 52]; Mtume ametumwa na Mwenyezi Mungu (swt) akiwa na sharia iliyorudiwa tena au mpya ambayo anawalingania watu, huku Nabii ametumwa na Mwenyezi Mungu (swt) kuthibitisha sharia ya iliyopita.” Hivyo, Musa (as) alikuwa Nabii kwa sababu alipewa wahyi kwa Shari´ah na ni Mtume kwa sababu Shari´ah hii ilikuwa kwa ajili ya utume wake. Kwa upande mwingine, ingawa Harun (as) pia alikuwa Nabii kwa sababu alipewa wahyi na Shari’ah, hakuwa Mtume kwa sababu Shari’ah, iliyoteremshwa kwake, haikuwa kwa ajili ya utume wake; bali ilikuwa ni kwa ajili ya utume wa Musa (as). Kwa mantiki hiyo hiyo, Muhammad (saw) alikuwa Nabii na Mtume kwa sababu alipewa wahyi na Shari’ah, ambayo ilikuwa kwa ajili ya utume wake]. **Mwisho wa nukuu.**

Rai hii ndiyo sahihi zaidi ya maneno na ndiyo inayowezekana zaidi kuwa sahihi. Hadith za Mtume (saw) zinaeleza uhalisia wa Nabii na tofauti kati yake na Mtume. Kwa mfano, Hadith iliyopokewa na Bukhari na Muslim kutoka kwa Abu Hazim, alisema: Nilikaa na Abu Huraira

***Endelea... UK 7***

miaka mitano, basi nikamsikia akisema kuwa Mtume amesema.

**كَانَتْ بَنُو إِسْرَائِيلَ تَسُوسُهُمْ الْأَنْبِيَاءُ كُلَّمَا هَلَكَ نَبِيٌّ خَلَفَهُ نَبِيٌّ، وَإِنَّهُ لَا نَبِيَّ بَعْدِي، وَسَيَكُونُ خُلَفَاءُ فَيَكْثُرُونَ. قَالُوا: فَمَا تَأْمُرُنَا؟ قَالَ: فُوا بِبَيْعَةِ الْأَوَّلِ فَالْأَوَّلِ؛ أَعْطُوهُمْ حَقَّهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ سَائِلُهُمْ عَمَّا اسْتَرْعَاهُمْ**

**"Walikuwa wana wa Isra'il siasa zao zikiendeshwa na Manabii, kila Nabii alipokufa alirithiwa na Nabii mwengine. Na hakika yake hakutakuwa na Nabii mwengine baada yangu, lakini watakuwepo makhalifa na watakuwa wengi."** Akaulizwa watuamrisha nini? Akasema, **"Mpeni ahadi ya utiifu (Bay'ah) mmoja baada ya mmoja; na wapeni haki yao kwani Mwenyezi Mungu atawauliza yale aliyowapa uchungaji kwayo."**

Ni wazi kutokana na Hadith hii kwamba Manabii wa Wana wa Israil ndio waliokuwa wakiwatawala, na hilo lilikuwa ni kwa mujibu wa Shariah ya Musa (as) kama inavyojulikana na inavyoonyeshwa na Hadith yenyewe, kwani inafananisha maumbile ya kazi ya makhalifa kwa kazi ya Manabii wa wana wa Israili, yaani, katika masuala ya utawala wa watu. Kama vile Manabii wa Wana wa Israili walivyokuwa wakiwatawala watu kwa mujibu wa Shariah ya Musa (as), ndivyo walivyo makhalifa; pia wanatawala Waislamu kwa mujibu wa Shariah ya Muhammad (saw). Hii ina maana kwamba Manabii wa wana wa Israili hawakuja na Shariah mpya, bali walifuata Shariah ya Musa (as). Hadith hii inaashiria kuwa Nabii ndiye anayepokea wahyi na kuwafahamisha watu juu yake, lakini hawajulishi sharia mpya; bali anafikisha Shariah ya Mtume aliyetangulia. Na kutokana na hilo pia inafahamika kwamba Mtume ndiye anayeleta Shariah mpya ambayo Manabii wanaomfuata wanaweza kuifuata, kama ilivyo kwa Manabii wa Wana wa Israili kuhusiana na Musa (as). Hadith iliyotajwa hapo juu ni ushahidi wa uhalisia wa tofauti kati ya Nabii na Mtume.

**Pili: Uhalisia wa Bwana wetu Harun (as):**

1- Kama tulivyotaja katika andiko lililonukuliwa hapo juu kutoka katika kitabu, Shakhsiya ya Kiislamu, tulisema: [Hivyo, Musa (as) alikuwa Nabii kwa sababu alipewa wahyi kwa Shari'ah na Mtume kwa sababu Shari'ah hii ilikuwa kwa ajili ya utume wake. Kwa upande mwingine, ingawa Harun (as) pia alikuwa Nabii kwa sababu alipewa wahyi na Shari'ah, hakuwa Mtume kwa sababu Shari'ah, iliyoteremshwa kwake, haikuwa kwa ajili ya utume wake; bali ilikuwa ni kwa ajili ya utume wa Musa (as)]. Kwa hiyo kwa kuzingatia ufafanuzi unaoelekea kuwa sahihi zaidi kwetu wa Nabii na Mtume, tumeamua kwamba Harun (as), ni Nabii na sio Mtume kwa maana hii, kwa sababu Harun (as), alikuwa akimfuata Musa (as) katika Shariah, na maandiko ya Shariah yanashuhudia hilo kama inavyoonyeshwa hapo chini.

2- Kuhusiana na aya mbili tukufu ulizozitaja katika swali, hebu tuziangalie tafsiri yake kwa ufupi kutoka katika baadhi ya vitabu vya tafsiri:

a- [Tafsir al-Nasafi (2/297, iliyohesabiwa moja kwa moja na al-Shamilah)

**فَأْتِيَاهُ "Basi mwendeeni"** yaani, kwa Firauni,**فَقُولا إِنَّا رَسُولاَ رَبّكَ "na mwambieni: Hakika sisi ni Mitume wa Mola wako Mlezi"** kwako wewe. Basi, wakenda kwake na kumfikishia Ujumbe na wakamwambia wameamrishwa kufanya hivyo.

**قَالَ فَمَن رَّبُّكُمَا يا موسى "(Firauni) akasema: Basi Mola wenu Mlezi ni nani, ewe Musa?"** Aliwahutubia, kisha akamwita mmoja wao, kwa sababu Musa ndiye mwenye asili ya utume, na Harun akamfuata...].

Imekuja pia katika [Tafsir al-Nasafi (2/ 464, iliyohesabiwa moja kwa moja na al-Shamilah)
**فَأْتِيَا فِرْعَوْنَ فَقُولا إِنَّا رَسُولُ رَبِّ الْعَالَمِينَ "Basi mfikieni Firauni na mwambieni: Hakika sisi ni Mitume wa Mola Mlezi wa walimwengu wote."** Mtume haikutumika muundo wa mbili (tathniya) kama ilivyo katika aya: **إِنَّا رَسُولاَ رَبّكَ "Hakika sisi ni Mitume wa Mola wako Mlezi"**

Kwa sababu Mtume inaweza kumaanisha yule aliyetumwa na inaweza kumaanisha Ujumbe, hivyo wakati mwingine ni katika maana ya yule anayetumwa, kwa hivyo hakuna haja ya kuzifanya katika muundo wa tathniya (mbili). Hapa ni katika maana ya Ujumbe; kwa hiyo, ni sawa katika maelezo ya moja, mbili au wingi. Au kwa sababu wameungana na kuafikiana katika Shariah moja kana kwamba wao ni Mtume mmoja. Au nataka kila mmoja wetu **[أَنْ أَرْسِلْ] "atume"** maana ya kutuma, ili Mtume ajumuishe maana ya kutuma na iwe na maana ya usemi **[مَعَنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ] "Pamoja nasi wana wa Israail"**. Anamaanisha kuwaacha waende nasi Palestina na yalikuwa makaazi yao. Basi wakaja mlangoni kwake, ruhusa haikutolewa kwa muda wa mwaka mmoja, mpaka mlinzi wa mlango akasema: Kuna mtu hapa anayedai kuwa ni Mtume wa Mola Mlezi wa walimwengu wote. Akasema: Mruhusu ili tumcheke. Basi wakampa Ujumbe, na Firauni akamjua Musa...]

b- [Tafsir Al-Qurtubi (13/93) kauli ya Mwenyezi Mungu (swt): **فَأْتِيَا فِرْعَوْنَ فَقُولا إِنَّا رَسُولُ رَبِّ الْعَالَمِينَ "Nendeni kwa Firi'aun na mkamwambie: 'Tuna ujumbe wa Mola Mlezi wa walimwengu wote."** Abu Ubaidah akasema: Mtume anaweza kuwa katika maana zote mbili maana ya uwili na wingi. Waarabu husema: Huyu ni mjumbe wangu na msaada wangu, na hawa wawili ni Wajumbe wangu na nguzo yangu, na hawa (wengi) ni Wajumbe wangu na nguzo yangu. Miongoni mwa haya ni kauli ya Mwenyezi Mungu (swt): **فَإِنَّهُمْ عَدُوٌّ لِي "Kwa kuwa wao ni maadui zangu"**. Na ikasemwa: Maana yake ni kuwa kila mmoja wetu ni Mtume wa Mola Mlezi wa walimwengu wote].

c- Kwa kuzichunguza Aya hizi mbili na Aya nyenginezo ambamo Harun (as) ametajwa kwa neno al-irsal (kutumwa) na al-Risala (ujumbe), inadhihirika kuwa kumtaja kwa neno al-irsal ilikuwa daima. pamoja na Musa (as), yaani, kwa kumfuata, kwa mfano kauli yake Mwenyezi Mungu isemayo: **ثُمَّ أَرْسَلْنَا مُوسَى وَأَخَاهُ هَارُونَ بِآيَاتِنَا وَسُلْطَانٍ مُبِينٍ "Kisha tukamtuma Musa na ndugu yake Harun pamoja na aya zilizo wazi"** [Al-Mu'minun: 45]

**وَأَخِي هَارُونُ هُوَ أَفْصَحُ مِنِّي لِسَاناً فَأَرْسِلْهُ مَعِيَ رِدْءاً يُصَدِّقُنِي إِنِّي أَخَافُ أَنْ يُكَذِّبُونِ "Na ndugu yangu Harun ni fasihi zaidi ulimi wake kuliko mimi. Basi mtume ende nami kunisaidia, ili anisadikishe. Hakika mimi nina khofu watanikadhibisha."** [Al-Qasas: 34]

***Endelea... UK 8***

وَإِذْ نَادَى رَبُّكَ مُوسَى أَنِ ائْتِ الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ * قَوْمَ فِرْعَوْنَ أَلَا يَتَّقُونَ * قَالَ رَبِّ إِنِّي أَخَافُ أَنْ يُكَذِّبُونِ * وَيَضِيقُ صَدْرِي وَلَا يَنْطَلِقُ لِسَانِي فَأَرْسِلْ إِلَى هَارُونَ * وَلَهُمْ عَلَيَّ ذَنْبٌ فَأَخَافُ أَنْ يَقْتُلُونِ * قَالَ كَلَّا فَاذْهَبَا بِآيَاتِنَا إِنَّا مَعَكُمْ مُسْتَمِعُونَ * فَأْتِيَا فِرْعَوْنَ فَقُولَا إِنَّا رَسُولُ رَبِّ الْعَالَمِينَ * أَنْ أَرْسِلْ مَعَنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ

**“Na Mola wako Mlezi, alipo mwita Musa, akamwambia: Fika kwa watu madhaalimu * Watu wa Firauni. Hawaogopi? * Akasema: Hakika mimi nachelea wasinikanushe * Na kifua changu kina dhiki, na ulimi wangu haukunjuki vyema. Basi mtumie ujumbe Harun * Na wao wana kisasi juu yangu, kwa hivyo naogopa wasije kuniuwa * Akasema: Siyo hivyo kabisa! Nendeni na miujiza yetu. Hakika Sisi tu pamoja nanyi, tunasikiliza * Basi mfikieni Firauni na mwambieni: Hakika sisi ni Mitume wa Mola Mlezi wa walimwengu wote * Waachilie Wana wa Israili wende nasi.”** [Ash-Shu’ara: 10-17]

اذْهَبْ أَنْتَ وَأَخُوكَ بِآيَاتِي وَلَا تَنِيَا فِي ذِكْرِي * اذْهَبَا إِلَى فِرْعَوْنَ إِنَّهُ طَغَى * فَقُولَا لَهُ قَوْلاً لَيِّناً لَعَلَّهُ يَتَذَكَّرُ أَوْ يَخْشَى * قَالَا رَبَّنَا إِنَّنَا نَخَافُ أَنْ يَفْرُطَ عَلَيْنَا أَوْ أَنْ يَطْغَى * قَالَ لَا تَخَافَا إِنَّنِي مَعَكُمَا أَسْمَعُ وَأَرَى * فَأْتِيَاهُ فَقُولَا إِنَّا رَسُولَا رَبِّكَ فَأَرْسِلْ مَعَنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ وَلَا تُعَذِّبْهُمْ قَدْ جِئْنَاكَ بِآيَةٍ مِنْ رَبِّكَ وَالسَّلَامُ عَلَى مَنِ اتَّبَعَ الْهُدَى * إِنَّا قَدْ أُوحِيَ إِلَيْنَا أَنَّ الْعَذَابَ عَلَى مَنْ كَذَّبَ وَتَوَلَّى

**“Nenda, wewe na ndugu yako, pamoja na ishara zangu, wala msichoke kunikumbuka * Nendeni kwa Firauni. Hakika yeye amepindukia mipaka * Mwambieni maneno laini, huenda akazingatia au akaogopa * Wakasema: Ewe Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tunaogopa asije akapindukia mipaka juu yetu au kufanya jeuri * Akasema: Msiogope! Hakika Mimi ni pamoja nanyi. Nasikia na ninaona * Basi mwendeeni, na mwambieni: Hakika sisi ni Mitume wa Mola wako Mlezi! Basi waache Wana wa Israili watoke nasi, wala usiwaadhibu. Sisi tumekuletea ishara itokayo kwa Mola wako Mlezi. Na amani itakuwa juu ya aliye fuata uwongofu * Hakika tumefunuliwa sisi kwamba hapana shaka adhabu itamsibu anaye kadhibisha na akapuuza.”** [Ta-Ha: 42-48]. Ni wazi kutokana na nususi zote hizi kwamba Harun (as) hakuwa peke yake katika maelezo ya Ujumbe; bali, maelezo yalikuwa juu ya Musa na juu yake pamoja, amani iwe juu yao wote wawili, ikimaanisha kwamba Harun (as), hakuwa huru na wa kipekee katika maelezo ya Ujumbe.

d- Lakini pale Harun (as) anapotajwa ndani ya Qur’an Tukufu huru peke yake katika maelezo, aliitwa Nabii na sio Mtume, na huu ni wakati ambao Qur’an ilimthibitisha Musa (as) sifa ya Mtume na Nabii kwa pamoja, Mwenyezi Mungu (swt) asema:

**“Na mtaje Musa katika Kitabu. Hakika yeye alikuwa ni mwenye kuchaguliwa, na alikuwa Mtume, Nabii * Na tulimwita upande wa kulia wa mlima na tukamsogeza kunong'ona naye * Nasi kwa rehema zetu tukampa nduguye, Harun, awe Nabii.”** [Maryam: 51-53] Yeye (swt) amesema kuhusu Musa (as) kwamba yeye alikuwa: رَسُولًا نَّبِيًّا **“alikuwa Mtume na Nabii”** [Maryam: 51] Ama Harun (as), mara tu baada ya hilo, Qur’an haikuthibitisha maelezo ya Ujumbe, lakini ilitosheleza kumsifia kwa unabii: أَخَاهُ هَارُونَ نَبِيّاً **“nduguye, Harun, awe Nabii.”** [Maryam: 53]. Hili linaunga mkono ufahamu wetu kwamba Musa (as) ni Nabii na Mtume, kwa sababu Shariah mpya ilitumwa kwake na akaamrishwa kuifikisha. Ama Harun (as) yeye ni Nabii wala si Mtume kwa sababu alimfuata Musa (as) na akaamrishwa kufikisha Ujumbe wa Musa (as), na Shariah yake bila ya kuwa na Shariah mpya inayojitegemea. Yafuatayo yameelezwa katika tafsiri ya aya hizi katika Ibn Kathir:

**[Tafsir Ibn Katheer (5/237) ...Pindi Mwenyezi Mungu (swt) alipomtaja Ibrahim Al-Khalil na kumsifu, Al-Kaleem Alitaja, na kusema:** وَاذْكُرْ فِي الْكِتَابِ مُوسَى إِنَّهُ كَانَ مُخْلَصاً **“Na mtaje Musa katika Kitabu. Hakika yeye alikuwa ni mwenye kuchaguliwa”** [Maryam: 51].

وَكَانَ رَسُولا نَبِيّاً **“na alikuwa Mtume na Nabii”** [Maryam: 51] **Sifa mbili ziliunganishwa kwa ajili yake,** kwa sababu alikuwa miongoni mwa Mitume watukufu watano (Uli Al-Azam), nao ni: Nuh, Ibrahim, Musa, Isa na Muhammad, rehma na amani ziwashukie wao na Manabii wote waliosalia... Na kauli yake: وَوَهَبْنَا لَهُ مِنْ رَحْمَتِنَا أَخَاهُ هَارُونَ نَبِيّاً **“Nasi kwa rehema zetu tukampa nduguye, Harun, awe Nabii.”** [Maryam: 53]. Ikimaanisha: Tulijibu dua na ombi lake kwa kaka yake, hivyo tukamfanya Nabii, kama alivyosema katika aya nyengine

وَأَخِي هَارُونُ هُوَ أَفْصَحُ مِنِّي لِسَاناً فَأَرْسِلْهُ مَعِيَ رِدْءاً يُصَدِّقُنِي إِنِّي أَخَافُ أَنْ يُكَذِّبُونِ **“Na ndugu yangu Harun ni fasihi zaidi ulimi wake kuliko mimi. Basi mtume ende nami kunisaidia, ili anisadikishe. Hakika mimi nina khofu watanikadhibisha.”** [Al-Qasas: 34]. Mwenyezi Mungu (swt) asema: قَدْ أُوتِيتَ سُؤْلَكَ يَا مُوسَى **“Hakika Umepewa maombi yako, ewe Musa!”** [Ta-Ha: 36] Mwenyezi Mungu (swt) asema: فَأَرْسِلْ إِلَى هَارُونَ * وَلَهُمْ عَلَيَّ ذَنْبٌ فَأَخَافُ أَنْ يَقْتُلُونِ **“Basi mtumie ujumbe Harun * Na wao wana kisasi juu yangu, kwa hivyo naogopa wasije kuniuwa.”** [Ash-Shu’ara: 13-14].

Ndio maana baadhi ya waliotangulia walisema: Hakuna aliyepewa uombezi duniani kuliko uombezi wa Musa kwa Harun, kwamba yeye awe Nabii. Mwenyezi Mungu (swt) asema: وَوَهَبْنَا لَهُ مِنْ رَحْمَتِنَا أَخَاهُ هَارُونَ نَبِيّاً **“Nasi kwa rehema zetu tukampa nduguye, Harun, awe Nabii.”** [Maryam: 53] Ibn Jarir amesema: Ya'qub alituambia, Ibn Aliyah alituambia, kutoka kwa Daud, kutoka kwa Ikrimah, alisema: Ibn Abbas alisema: Kauli yake. وَوَهَبْنَا لَهُ مِنْ رَحْمَتِنَا أَخَاهُ هَارُونَ نَبِيّاً **“Nasi kwa rehema zetu tukampa nduguye, Harun, awe Nabii.”** [Maryam: 53] Akasema: Harun alikuwa mkubwa kuliko Musa, lakini alitaka kumpa unabii wake].

3-Kutokana na yaliyotajwa hapo juu, inadhihirika kuwa kwa mujibu wa ufafanuzi tunaouchukua wa Nabii na Mtume, Musa (as), ni Nabii kwa sababu iliteremshwa Shariah ili kuifikisha, na Mtume kwa sababu Shariah maalum iliteremshwa kwake. Ama Harun (as) ni Nabii kwa sababu aliteremshiwa Shariah, lakini yeye si Mtume kwa sababu Shariah iliyoteremshwa kwake kufikisha haikuwa makhsusi kwake; bali ilikuwa ni Shariah makhsusi kwa kaka yake Musa (as).

Haya ndiyo tunayoyaona kuwa ndiyo rai iliyo sahihi katika jambo hili, nayo ndio rai yetu iliyotabanniwa, na Mwenyezi Mungu (swt) ni Mjuzi Zaidi na Mwingi wa hekima.

**Ndugu Yenu,**

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**
**12 Shawwal 1444 H**
**2/5/2023 M**